




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI**  
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Email [ded@babatidc.go.tz](mailto:ded@babatidc.go.tz)

Website: [www.babatidc.go.tz](http://www.babatidc.go.tz)

S.L.P 400  
**BABATI,**

Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. DED/BBT/B.30/22

22/07/2024

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa idhini ya Kamati ya Fedha na Uongozi anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi Katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati vituo vya Afya vya Bashnet, Magugu, Gidas, Magara na Hospitali ya Mwada kuomba nafasi za kazi tajwa hapo chini kwa masharti ya muda na kuhuishwa mkataba kwa ufanisi wa kazi kama ifuatavyo:

### 1.0 MSAIDIZI WA HESABU DARAJA II (NAFASI 5)

#### 1.1 Sifa za Waombaji

Waombaji wawe wamehitimu kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) wenye Astashahada (Certificate) ya katika mojawapo ya fani za Uhasibu, Cheti cha ATEC level II au "Foundation Level" kinachotolewa na NBAA, waombaji wawe na uzoefu wa kazi angalau mwaka (1) katika fani hiyo.

#### 1.2 Majukumu ya Kazi

- i. Kuandika na kutunza "Register" zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- ii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha.
- iii. Kutunza majalada yenyewe kumbukumbu za hesabu.
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki.
- v. Kufanya usuluhisho kwa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana.
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazo pangwa na Mwajiri wake.

#### 1.3 Ngazi ya Mshahara ni kwanza kuzingatia viwango vya Serikali yaani **TGS B<sub>1</sub>** kwa mwezi.

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi m, iaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini.
- ii. Waombaji wenyе ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye aina ya ulemavu alionao kwa ajili ya taarifa.
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenyе anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (Email address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji wwatakao wasilisha taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
- v. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati S.L.P 400 Babati au kwa mkono Masijala ya Mkurugenzi iliyopo Makao Makuu Arri.
- vi. Maombi yatakayowasilishwa kinyume au nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.
- vii. Hati za matokeo havitatambulika (Testimonials and Provisional results).
- viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa mkono.
- ix. Waombaji waliosomea nje ya wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU au NECTA) ya Tanzania.
- x. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **30 Julai, 2024 saa 09:30 Alasiri**.

Tangazo hii limetolewa na



Nakala; Mbao za Matangazo